

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Telegrams: "UTUMISHI", DAR ES SALAAM
Tel. No. : +(255) 22 2118531-4
Fax No.: +(255) 22 2125299
E-mail: permsec@utumishi.go.tz



OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA,
JENGO LA UTUMISHI,
8 BARABARA YA KIVUKONI,
S.L.P. 2483,
11404 DAR ES SALAAM.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. EG. 45/86/01/"D"/ 48

07 Oktoba, 2015

Makatibu Wakuu Wote,
Wakuu wa Idara Zinazojitegemea Wote,
Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali Wote,
Makatibu Tawala wa Mikoa Wote,
Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Miji Wote,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya Wote.

YAH: UTEKELEZAJI WA AHADI YA UADILIFU KWA WATUMISHI WA UMMA

Tafadhali rejea somo hilo hapo juu.

2. Pamoja na barua hii, nawasilisha kwenu Nakala ya *Fomu ya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma* pamoja na Nakala ya *Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.2 wa mwaka 2015* kuhusu utekelezaji wa ujazaji wa Fomu ya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma. Nakala za Fomu ya Ahadi ya Uadilifu na Waraka tajwa zinapatikana kupitia Tovuti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma – www.utumishi.go.tz. Utaratibu wa kukutumia Nakala ngumu (hard copy) unaandaliwa na Ofisi yangu kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi.

3. Ili kutekeleza suala hili kwa ukamilifu, Waajiri wanashauriwa kutenga muda au siku maalum ya kutekeleza agizo hili, kuwawezesha watumishi katika makundi tofauti kupata fursa ya kupitia kwa pamoja maelezo yaliyomo katika fomu hii ya Ahadi ya Uadilifu na kisha kusaini. Baada ya kusaini, nakala moja atakabidhiwa Mtumishi na nakala nyingine itawekwa kwenye jalada lake binafsi. Zoezi hili litaendelea kufanyika kila mwaka kwa watumishi wa Umma wote.

4. Ni jukumu la Wizara, Ofisi na Taasisi nyingine kuhakikisha kuwa Taasisi na Ofisi zote zilizopo chini yake zinatekeleza agizo hili kwa ukamilifu. Pia mnatakiwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa suala hili mwezi Juni

kila mwaka ili kuiwezesha Ofisi yangu kuratibu utekelezaji wa agizo hili kama ilivyoelekezwa katika Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 2 wa mwaka 2015 aya ya 4(4.1)(b) na 7.

5. Tafadhali mnaombwa kukiri kupokea barua hii ili kuweka kumbukumbu sahihi.

Nawashukuru kwa ushirikiano wenu.


HAB Mkwizu

KAIMU KATIBU MKUU (UTUMISHI)

Nakala: 1. Katibu Mkuu Kiongozi,
Ofisi ya Rais - IKULU,
S.L.P 9120,
DAR ES SALAAM.

2. Kamishna,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma,
Mtaa wa Ohio,
S.L.P 1334,
DAR ES SALAAM.

